

IMF YARIDHISHWA NA UKUAJI WA UCHUMI KATIKA SERIKALI YA TANZANIA

Shirika la Fedha Duniani (IMF), limeridhishwa na jitihadi za serikali ya Tanzania katika kukuza uchumi, hayo yalisemwa na mwakilishi mwandamizi wa IMF, David Robinson alipositiza kuwa Tanzania ina uwezo wa kukopa kwa kuwa haina madeni makubwa ya nje.

Waziri wa Fedha na Uchumi Mh. Mustafa Mkulo alieleza kuwa Shirika hili limekuwa likisaidia Tanzania katika suala zima la kukuza uchumi na kuifanya Tanzania kuweza kukabili na mtikisiko wa uchumi. Aidha Mh. Waziri aliishukuru IMF kwa jitihada za kufuatilia mwenendo wa uchumi wa Tanzania na akaahidi kuwa serikali yake itaendelea kuboresha sera za uchumi, pia alipata fursa ya kumkabidhi mwakilishi wa shirika hili la Misaada Tanzania tunzo ya utendaji bora wa kazi Bi. Mita Samat ambaye ni Meneja wa Ofisi wa IMF Tanzania.

Bw. David Robison alieleza kuwa, Lengo la IMF lilikuwa ni kuona uchumi wa Tanzania angalau unakua kwa asilimia 5, “nafahamu kuwa mfumuko wa bei ulikuwa umepanda na kufikia asilimia 15 lakini kutokana na juhudi za serikali zinazoendelea kufanywa kupitia kilimo hali inaonesha mwelekeo ni nzuri” alisisitiza.

Pamoja na IMF kutoa fursa hiyo kwa Tanzania, Robinson alisema inatakiwa kuwa na uangalifu katika ukopaji wake kwa maana ya kutokopa sana.

Waziri wa fedha na Uchumi Mustafa Mkulo aliishukuru IMF kwa hatua waliyofikisha na kulidhibitishia shirika hilo kwamba Tanzania ipo tayari na imejipanga vizuri kusimamia uchumi na taasisi zake za kifedha.

IMETOLEWA NA MSEMAJI MKUU

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

18/03/2010